# WASIFU WA MZEE HAMISI AKIDA

*Sihiyana Salehe (Mandevu)*
*na*
*V.G. Nkondokaya*

Mzee Hamisi Akida alizaliwa Tanga tarehe 22/11/1914. Amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 94.

Katika uhai wake, Mzee Akida alikuwa mbele katika kuendeleza Kiswahili. Alikuwa mpenzi, mwanachama, mwanataaluma na gwiji la Kiswahili; kuanzia wakati wa uhai wa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika ya Mashariki mwaka 1930, Halmashauri ya Kiswahili hapo mwaka 1954 na TUKI mwaka 1972. Hadi anastaafu, Mzee Akida alikuwa mfanyakazi wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baadaye UKUTA ambako alistaafu kutokana na maradhi.

**Maisha yake kwa Ufupi**

Mzee Akida aliishi Tanga, Tabora (alisoma) halafu alikuja Dar es Salaam kufanya kazi. Amefanya kazi pia (ukarani) huko Mahenge, Mafia, Utete (Rufiji), Morogoro na Kisarawe.

Baba yake alikuwa Mdigo ambaye aliitwa Akida Mimi. Kama ilivyo kwa watu wa Tanga (pwani) jina hilo alilipata kutokana na kujinasabisha sana na umaarufu ambao hata hivyo, unapatikana kwa taabu kubwa ikiwa ni pamoja na kutoa mali na pesa nyingi; alipofanikiwa ndipo akajiita Akida Mimi.

Mama yake mzazi aliitwa Amina. Mama huyu ni uzao wa ukoo wa Wakilindi (ukoo ambao mwasisi wake ni Mbega).

Mke wake wa kwanza ni Majuto Binti Kombo. Huyu alizaa naye watoto watatu ambao ni Salama, Akida na Kombo (ambaye sasa ni marehemu). Mke wa pili anaitwa Hatnafsi Athumani, huyu amezaa naye watoto wanne ambao ni Kudra (ambaye sasa ni marehemu), wengine ni Abdu, Ayubu na Hassan (ambaye ndiye kitinda mimba). Mke wa tatu **[JINA?]** hakuzaa naye.

Marafiki zake wa karibu walikuwa ni *Washairi, wanamuziki wa taarabu*, wapenzi wa Kiswahili na umma wote kwa ujumla. Kuhusu michezo na burudani, Mzee Akida alikuwa mcheza mpira wa miguu na amewahi kuchezea timu ya Sunderland (sasa Simba Sports Club), baadaye alihamia timu ya *Yanga Afrikans* ambako alikuwa mpenzi, mwanachama, mshauri na rafiki wa karibu wa viongozi wa timu hii. Mzee Akida pia alikuwa wanamuziki na alikuwa mpiga kinanda wa kikundi cha taarabu cha Egyptian. Mwimbaji mkuu wa kikundi hiki

enzi hizo alikuwa ni Abbas Mzee. Makao ya klabu hii yalikuwa kati ya mitaa ya Lumumba na Ungoni.

**Umaarufu wa Mzee Akida**

Mzee Akida alikuwa maarufu katika mambo mengi, hapa tutataja moja kati ya umaarufu ambao ameupata. Majengo na eneo lote la Arnatouglo, Mnazi Mmoja, Dar es Salaam ni mfano mkubwa wa umaarufu wake. Akiwa Diwani wa Dar es Salaam ndiye aliyefanya juhudi hadi kuwepo kwa majengo haya leo hii.

Baada ya Karimjee (tajiri wa Kihindi) kujenga majengo maarufu yaliyopewa majina yake, wenyeji nao (yaani Waafrika) walipenda wajengewe jengo lao ambalo wangelitumia kwa starehe na kupumzika; baadhi ya watu walipenda lijengwe pale ambapo leo ipo Baa kubwa maarufu inayoitwa DDC Kariakoo, wengine walipenda lijengwe maeneo ya Upanga. Wenyeji wengi hawakupenda jengo hilo lijengwe Upanga kwani hawakai huko. Baada ya mvutano mkubwa Mzee Akida akafanya juhudi kubwa na kupata eneo yalipo majengo haya leo hii. Hata hivyo, kulikuwa na taabu ya kupata mfadhili; kwa bahati, katika kamati ya Mzee Akida ya kushughulikia suala hili alikuwepo mwanakamati mmoja ambaye alikuwa rafiki wa tajiri mkubwa Mgiriki ambaye hata hivyo, shughuli zake alikuwa anazifanyia katika nchi ambayo leo inajulikana kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC). Mgiriki huyu alikubali kusaidia, hivyo kwa sababu jina lake aliitwa "Arnatouglo" mahali hapo pameitwa jina hili hadi leo.

**Vyuo/Shule/Kozi Alizochukua**

Katika maisha yake Mzee Akida amehudhuria mafunzo na kazi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Elimu ya Sekondari, Tanga - 1932
- Kozi ya Ukarani, Tabora - 1934
- Programu ya Mtihani NEC - 1942
- *Matric Certificate*, Cape Town, Afrika ya Kusini - 1944-46
- *Public Administration Course, Nairobi*, Kenya - 1952-54
- Kozi Maalumu ya Uongozi, DSM - 1964
- Mwanachama wa Kamati ya Elimu ya Dini ya Kiislamu - 1950-52
- Karani wa Daraja la Juu, Ofisi ya Utawala ya Mkoa, DSM 1951-60
- Mfanyakazi wa Ofisi, Wizara ya Habari - 1960-62
- Msimamizi wa Ofisi, Ofisi ya Rais, DSM - 1962-66

**Kazi Alizofanya Tuki, Chuo Kikuu cha DSM**

Akiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mzee Akida alifanya kazi zifuatazo:-

- Mtafiti Msaidizi - 1970
- Mtafiti Mwandamizi Msaidizi - 1974
- Mtafiti Mwandamizi - 1976
- Mchunguzi Mwandamizi - 1978

Kazi hizi amezifanya akiwa katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**Kazi na Shughuli Nyingine**

Mbali na kazi alizokuwa anafanya TUKI, pia Mzee Akida alifanya shughuli nyingine muhimu kama:-

- Kufundisha Kiswahili kwa Wanafunzi wa Kigeni
- Kiongozi wa Shina, CCM
- Mwenyekiti BAKIJI (Baraza la Kiswahili la Jiji, DSM)
- Kushiriki katika vipindi vya Redio Tanzania kuhusu Kiswahili (Mbinu za Kiswahili)
- Amehudhuria mikutano mingi ya *International Standardization Organization (ISO* = Chama cha Kimataifa cha Usanifishaji) kuhusu istilahi
- Mtoa mada katika redio kuhusu chimbuko/asili ya majina mbalimbali, mfano majina ya maeneo ya Dar es Salaam.

**Baadhi ya Kazi zake za Uandishi**

Mzee Akida pia alikuwa mwandishi mashuhuri. Baadhi ya kazi zake ni kama ifuatavyo:-

- Mwanajopo, Mwanaleksikografia, mmoja wa watungaji na wahariri wa kamusi mashuhuri za TUKI kama vile *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili, (English-Swahili Dictionary)* na nyingine
- Mwenyekiti na mwanachama wa muda mrefu wa UKUTA (Chama cha Ushairi wa Kiswahili Tanzania)
- Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania: Istilahi (1986)
- *Swahili-English Pocket Dictionary* (Mkuki na Nyota Publishers 2003)
- Shughuli za Utengenezaji wa Msamiati wa Lugha
- *Terminology Activities in Tanzania* (katika *Tanzania Journal*) UJISLAA, Paris, 1981
- Msamiati wa Kibiolojia (1981)
- Kazi za Utengenezaji, Msamiati (TERMNET News, Vienna, 1982)
- Msimamizi kuhusu Msamiati wa Kitabibu katika Kiswahili

- Kutoa ushauri kwa watu mbalimbali, mfano wanafunzi na wageni kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili
- Mwanachama wa Chama cha Wafasiri Tanzania (CHAWATA)
- Marehemu pia ameandika makala mengi ya kitaaluma katika majarida ya TUKI ya *Mulika* na *Kiswahili*, *Zinduko* na mengine mengi ya ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

Amefariki akiwa na umri wa miaka 94. Amefia Dar es Salaam, eneo la Mkwajuni Kinondoni tarehe 12 Machi, 2008 na kuzikwa katika makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam, siku ya Alhamisi, tarehe 13 Machi, 2008 saa 10.00 jioni.

Hii ndiyo historia fupi ya Mzee Hamisi Akida mshairi, gwiji na mtalaamu wa Kiswahili, na mwandishi wa vitabu na makala.

Mungu Ailaze Roho Yake Mahali Pema Peponi, Amina*

* *Wasifu huu ulitolewa tarehe 3/5/2008 Ukumbi wa Arnatouglo, Mnazi Mmoja, Dar es Salaam, katika kumbukizi ya kuwakumbuka Mzee Hamisi Akida na Profesa Z.M.S. Mochiwa*